

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU



*Zanzibar*  
*13 Disemba, 2024*

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya uteuzi na kumpangia Balozi kituo cha kazi. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi Balozi Dkt. Moses Kusiluka, uteuzi huo ni:-

- (i) Bw. Majaba Shabani Magana ameteuliwa kuwa Kamishna wa Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu (FIU) akichukua nafasi ya Bi. Fatma Ayoub Mwinyimvua Simba. Kabla ya uteuzi huu, Bw. Magana alikuwa Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa Wateja Wakubwa, Benki ya Azania; na
- (ii) Balozi Selestine Gervas Kakele amepangiwa kuwa Balozi wa Tanzania nchini Nigeria. Balozi Kakele anachukua nafasi ya Balozi Dkt. Benson Alfred Bana ambaye amestaafu.

Sharifa B. Nyanga  
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu



*Ikulu Mawasiliano / ikulu\_mawasiliano /  
ikulu\_Tanzania / ikulu Tanzania /  
ikulumawasilano / Ikulu Tanzania / Ikulu Tanzania*



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**



*Ikulu Mawasiliano / ikulu\_mawasiliano /  
ikulu\_Tanzania / ikulu Tanzania /  
ikulumawasilano / Ikulu Tanzania / Ikulu Tanzania*

